

# MAELEKEZO



# ZIWANI



**USIWARUHUSU WATOTO WAENDE ZIWANI BILA WATU WAZIMA**

## **FUATILIA WATOTO KWENYE MAJI!**

Mtoto huweza kuzama katika sekunde chache, kimya. Kaa karibu na mtoto ndani ya maji kama umbali wa mkono wako. Mtoto awe kati yako na nchi kavu.

## **WAFUNDISHE WATOTO**

kwamba hawaruhusiwi kwenda majini au karibu na maji bila mtu mzima.

## **MTOTO ANAPOJIFUNZA KUOGEELEA**

na vitu vinavyoelea mikononi au na nguo za kuogeelea zinazoelea, vitu hivi huweza kutumika kwa mafunzo. Hata hivyo, kumbuka kwamba vitu hivyo si vifaa vya uokoaji. Mtoto asiyejua kuogeelea hapaswi kuachwa bila tahadhari.

## **HAKIKISHA KWAMBA SEHEMU ZIWANI NI SALAMA KWA KUOGEELEA AU KURUKA**

Kila mwaka, hata watu wanaojua kuogeelea vizuri huzama majini Ufini. Kuzama ni mojawapo ya sababu za kawaida za kifo cha ajali kwa watoto. Tafadhali jali usalama wako mwenyewe na usalama wa watoto wako

